VERMONT
DEPARTMENT OF HEALTH

Vital Records Office
Vermont Department of Health
280 State Dr,
Waterbury VT 05671-8370
802-863-7275 or 800-439-5008 (katika VT tu)

# Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu ya Mzazi

Tafadhali andika kwa njia inayosomeka.

| | | |
|---|---|---|
| *Mtoto* | 1. Jina la Mtoto (La Kwanza, La Kati, La Mwisho, Maneno yanayoandikwa baada ya jina la mwisho) | 2. Tarehe ya Kuzaliwa (mwezi/siku/mwaka) |
| | 3. Jiji au Mji, Kaunti na Jimbo Alipozaliwa | |
| *Kijeni Mzazi wa* | 4. Jina la Sasa la Kisheria la Mzazi (La Kwanza, La Kati, La Mwisho, Maneno yanayoandikwa baada ya jina la mwisho) | 5. Nambari ya Ustawi wa Jamii (Social Security) |
| | 6. Tarehe ya Kuzaliwa (mwezi/siku/mwaka) | 7. Mahali pa Kuzaliwa (Jimbo, Wilaya au Nchi ya Kigeni) |
| | 8. Anwani ya Barua ya Posta (Mtaa na Nambari, Jiji/Mji, Jimbo, Msimbo wa Eneo) | |
| *Kijeni Mzazi wa Anayedaiwa kuwa au Kijeni Anayedhaniwa kuwa* | Jaza na uwasilishe fomu hii kwa Ofisi ya Rekodi Muhimu ya Idara ya Afya ya Vermont pamoja na Fomu ya Kukubali kwa Hiari kuwa Mzazi (VAP) ili uondolewe haki na majukumu yote ya mzazi ya mtoto aliyeorodheshwa hapo juu. Usajili wa fomu hii utaondoa jina la anayedhaniwa kuwa mzazi au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni aliyeorodheshwa hapo chini na kulibadilisha na jina la mzazi aliyeorodheshwa kwenye VAP halali. | |
| | 9. Jina la Sasa la Kisheria la Anayedhaniwa kuwa Mzazi au Anayedaiwa kuwa Mzazi wa Kijeni (La Kwanza, La Kati, La Mwisho, Maneno yanayoandikwa baada ya jina la mwisho) | 10. Nambari ya Ustawi wa Jamii (Social Security) |
| | 11. Tarehe ya Kuzaliwa (mwezi/siku/mwaka) | 12. Mahali pa Kuzaliwa (Jimbo, Wilaya au Nchi ya Kigeni) |
| | 13. Anwani ya Barua ya Posta (Mtaa na Nambari, Jiji/Mji, Jimbo, Msimbo wa Eneo) | |

**Kauli za Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu**

| Herufi za kwanza za jina | Anayedhaniwa kuwa mzazi au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni lazima aandike herufi za kwanza za jina lake kwenye kila kauli iliyo hapo chini ili Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu ya Mzazi iwe halali. |
|---|---|
| | Nimesoma na ninaelewa maagizo yaliyotolewa na matokeo ya kisheria ya na haki na majukumu yanayotokana na kusaini fomu ya kuondolewa haki na majukumu. |
| | Ninaelewa kuwa nina haki ya kuzungumza na mwanasheria kabla ya kusaini. |

<table>
<tr><td rowspan="7">Kijeni Mzazi wa Anayedaiwa kuwa au Kijeni Anayedhaniwa kuwa</td><td colspan="3">Kauli za Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu (inaendelea)</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="2">Ninaelewa kuwa kukataa huku, pamoja na Fomu halali ya Kukubali kwa Hiari kuwa Mzazi wa Mtu Fulani, ni sawa na uamuzi wa kukata kuwa wewe si anayedhaniwa kuwa mzazi au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni na anayedhaniwa kuwa mzazi au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni ameondolewa haki na majukumu yote ya mzazi.</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="2">Ninasema kuwa sijakubali au kuamuliwa kuwa mzazi wa mtoto aliyetajwa Mtoto hapo juu.</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="2">Ninaelewa kuwa ninaweza kubatilisha fomu hii ya kuondolewa haki na majukumu ya mzazi kwa kuwasilisha Fomu ya Kubatilisha katika Ofisi ya Rekodi Muhimu ndani ya siku 60 baada ya fomu hii ya kuondolewa haki na majukumu ya mzazi kuwasilishwa na kukubaliwa.</td></tr>
<tr><td></td><td colspan="2">Ninaelewa kuwa baada ya siku 60 za kuwasilisha fomu ya kukubali kuwa mzazi na fomu ya kuondolewa haki na majukumu ya mzazi katika Ofisi ya Rekodi Muhimu, ikiwa inafaa, lazima nipate uamuzi wa mahakama unaobatilisha au unaopinga fomu ya kukubali kuwa mzazi au fomu ya kuondolewa haki na majukumu ya mzazi ili niweze kuondoa au kuandika jina la mzazi.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Nimesoma na ninaelewa taarifa iliyo katika Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu ya Mzazi (DOP). Nabainisha kuwa taarifa hiyo ni sahihi kadri ninavyojua na kuamini. Ninasaini DOP hii bila kulazimishwa, kutishiwa wala kushurutishwa kwa njia yoyote.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Sahihi ya Anayedhaniwa au Anayedaiwa kuwa Mzazi wa Kijeni</td><td>Tarehe Ilipotiwa Saini (mwezi/siku/mwaka)</td></tr>
<tr><td>Shahidi</td><td colspan="2">Saini ya Shahidi</td><td>Tarehe Ilipotiwa Saini (mwezi/siku/mwaka)</td></tr>
</table>

**Kwa Matumizi ya Ofisi ya Rekodi Muhimu Pekee**

**Tarehe Ilipopokewa: ________________________**

# Taarifa na Maagizo ya Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu ya Mzazi

**Anayedhaniwa au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni anapaswa kusoma taarifa na maagizo yote kwa makini kabla ya kujaza na kutia saini kwenye Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu ya Mzazi (DOP).**

Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu ya Mzazi ni fomu ya kisheria inayotiwa saini na anayedhaniwa au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni ili kubainisha kuwa mtu huyo anakataa dai lolote la kuwa mzazi wa mtoto huyu. Ikiwa mzazi ambaye ameolewa au aliyekuwa ameolewa zamani anadai kuwa mwenzi wake wa ndoa au mwenzi wake wa zamani (anayedhaniwa kuwa mzazi au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni) si mzazi wa mtoto na mzazi wa mtoto angependa kukubali kuwa mzazi wa mtoto huyu, basi mwenzi wake anaweza kujaza Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu ya Mzazi mbele ya shahidi.

Ili iwe halali, wazazi wote wawili wa mtoto lazima pia watie saini kwenye fomu ya Kukubali kwa Hiari kuwa Mzazi (VAP). VAP na DOP zinaweza kuwasilishwa kwa wakati tofauti au kwa wakati mmoja, lakini fomu hizo hazitakuwa halali isipokuwa kama zote zimewasilishwa kwenye Ofisi ya Rekodi Muhimu ya Idara ya Afya ya Vermont. DOP hii itatiwa saini na anayedhaniwa au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni anayetaka kuacha majukumu ya kuwa mzazi mbele ya shahidi.

**1. Mzazi Ambaye Ameolewa au Aliyekuwa Ameolewa Zamani**

Wakati mzazi ameolewa au alikuwa ameolewa ndani ya siku 300 baada ya kuzaliwa kwa mtoto, jina la mwenzi litaandikwa kwenye Cheti cha Kuzaliwa, ikiwa ni pamoja na wakati ambapo:

a. Huenda mwenzi si anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni.
b. Mzazi alikuwa ameolewa kisheria, na mtoto anazaliwa ndani ya siku 300 baada ya kusitishwa kwa ndoa (isipokuwa kama amri ya mwisho ya talaka inabainisha kuwa mwenzi wa ndoa si mzazi wa kibiolojia).

**2. Ikiwa DOP imejazwa hospitalini:**

Ikiwa DOP imejazwa na hospitali imepewa fomu hiyo kabla ya Cheti cha Kuzaliwa kuwasilishwa katika Ofisi ya Rekodi Muhimu, mzazi ataorodheshwa kama mzazi kwenye cheti cha kuzaliwa.

**3. Ikiwa DOP haijajazwa hospitalini:**

Ikiwa DOP hii haijajazwa kabla ya hospitali kuwasilisha Cheti cha Kuzaliwa katika Ofisi ya Rekodi Muhimu, mwenzi wa sasa au mwenzi wa zamani (anayedhaniwa kuwa mzazi) ataorodheshwa kama mzazi kwenye cheti cha kuzaliwa.

**4. Legal Citations: 15C V.S.A., Chapters 1, 3, and 4**

- "Anayetambuliwa kama mzazi" ni mtu aliye na uhusiano wa mzazi na mtoto kwa kuwasilisha Fomu ya Kukubali kwa Hiari kuwa Mzazi kwenye Ofisi ya Rekodi Muhimu.
- “Aliyetamkwa kuwa mzazi” ni mtu ambaye mahakama yenye mamlaka iliamua kuwa yeye ni mzazi wa mtoto.
- “Anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni” ni mtu anayedaiwa kuwa au anayedai kuwa mtu huyo ni, mzazi wa kijeni au anaweza kuwa mzazi wa kijeni wa mtoto ambaye wazazi wake

hawajaamuliwa. Neno hili linajumuisha anayedaiwa kuwa baba wa kijeni na anayedaiwa kuwa mama wa kijeni. Neno hili halihusu mtu anayedhaniwa kuwa mzazi, mtu ambaye haki zake za mzazi zimesitishwa au imebainishwa kuna hana haki ya kuwa mzazi au alichangaia tu katika uzazi ila si mzazi.

- “Mzazi anayekusudiwa” ni mtu, awe ameolewa au hajaolewa, ambaye anadhihirisha nia ya kuwa mzazi wa mtoto kisheria kwa sababu alisaidia katika uzazi au kulingana na makubaliano ya mzazi ambaye si wa kijeni.
- "Anayedhaniwa kuwa mzazi" ni mtu anayetambuliwa kuwa mzazi wa mtoto hadi hali hiyo ikataliwe au ithibitishwe katika kesi ya mahakama. Mtu anadhaniwa kuwa mzazi wa mtoto ikiwa:
    a. Mtu na mwanamke aliyemzaa mtoto wameoana na mtoto amezaliwa wakati wa ndoa; au
    b. Mtu na mwanamke aliyemzaa mtoto walikuwa wameoana na mtoto amezaliwa ndani ya siku 300 baada ya ndoa kusitishwa kutokana na kifo, kubatilishwa, talaka, kuvunjika au tamko la kuwa batili; au
    c. watu waliomzaa mtoto walioana baada ya kuzaliwa kwa mtoto na kuna wakati ambapo mtu huyo alidai kuwa mzazi wa mtoto na alikubali kuwa mzazi na ametajwa kama mzazi wa mtoto kwenye cheti cha kuzaliwa cha mtoto huyo.
    d. mtu huyo aliishi katika nyumba moja na mtoto kwa miaka miwili ya kwanza ya maisha ya mtoto, ikiwa ni pamoja na vipindi vya kutokuwepo kwa muda, na mtu huyo na mzazi mwingine wa mtoto walikuwa wanasema wazi kuwa huyo ni mtoto wa mtu huyo.

**5. Maagizo ya Kujaza Fomu ya Kuondolewa Haki na Majukumu ya Mzazi:**

- ▢ Anayedhaniwa kuwa mzazi au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni lazima asome na aandike herufi za kwanza za jina lake kwenye kauli zote zilizojumuishwa kwenye DOP.
- ▢ Anayedhaniwa kuwa mzazi au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni lazima atie saini kwenye DOP mbele ya shahidi na shahidi huyo lazima atie saini kwenye DOP.
- ▢ Anayedhaniwa kuwa mzazi au anayedaiwa kuwa mzazi wa kijeni anaweza kuwasilisha DOP iliyojazwa hospitalini kabla ya kuwasilisha Cheti cha Kuzaliwa au moja kwa moja katika Ofisi ya Rekodi Muhimu, kwa anwani ya barua ya posta iliyotolewa hapo chini:

  Vital Records Office<br>
  Vermont Department of Health<br>
  280 State Dr,<br>
  Waterbury VT 05671-8370

**Iwapo unahitaji usaidizi wa kuelewa haki na majukumu yenu kama wazazi na njia mbadala za, na matokeo ya, kusaini fomu hii, pigia simu Ofisi ya Vermont ya Usaidizi wa Malezi ya Mtoto: 1-800-786-3214.**